# PROGRAMU YA KITUO CHA WAZAZI CHA EDULOG

# MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA YA WAZAZI NA WALEZI

## KWA JUMLA

**S: Kituo cha Wazazi cha Edulog ni nini? Ninawezaje kujisajili ili kukitumia?**
J: Programu ya vifaa vya mkononi ya Kituo cha Wazazi kutoka Education Logistics, Inc. (Edulog) huwezesha wilaya ya shule kushiriki maelezo yaliyopangwa na halisi ya usafiri wa shule na wazazi na walezi. Programu hii inatoa maelezo mapya kuhusu saa na eneo lililopangwa la kituo cha basi cha wanafunzi. Inaweza kuonyesha mkao wa basi la shule na kukupa arifu punde basi likikaribia kituo cha basi. Ukiwa una modyuli ya Usafiri wa Wanafunzi ya Edulog, wazazi na walezi hupokea arifu wakati mwanafunzi wao anapotumia kadi ya ID kwenye kisomaji kadi cha RFID akipanda na kushuka basi.

Pakua Edulog Parent Portal kutoka Google Play Store au Apple App Store. Tafuta "Edulog Parent Portal" na uchague programu yenye basi nyeupe na mandharinyuma ya rangi ya zumaridi.

Ukishapakua programu, jisajili kwa kutumia anwani yako ya barua pepe.

**KUMBUKA: Programu nyingine mama ya Edulog, Parent Portal Lite, ina basi ya rangi ya zumaridi kwenye mandharinyuma nyeupe, kwa hivyo kuwa mwangalifu upakue programu sahihi. Kwa kutumia msimbo wa QR uliopigwa picha hapa utaweza kufikia programu sahihi.**

**S: Kuna toleo la Kihispania?**
J: Ndiyo. Ukishapakua programu, lugha inaweza kubadilishwa kutoka Kiingereza hadi Kihispania kwenye kichupo cha MIPANGILIO. Hakikisha umechagua HIFADHI ili uendelee kwa lugha unayopendelea.

**S: Je, ninapaswa kusajili kando kila mmoja wa watoto wangu?**
J: Sajili tu mara moja kwa wilaya ya shule yako. Usajili mmoja hukuwezesha kufikia maelezo ya wanafunzi wote ambao una maelezo yao ya usalama.

## KWA KUWA SASA UMESAKINISHA PROGRAMU - ANZA KUTUMIA

**S: Ninawezaje kumsajili mwanafunzi wangu katika Kituo cha Wazazi?**
J: Hii inafanyika kutoka kwa kichupo cha ORODHA YA WANAFUNZI kwa kuchagua ikoni ya "+" au kitufe cha ONGEZA MWANAFUNZI. Ili kumsajili mwanafunzi wako, lazima uwe na sehemu 5 za maelezo ili uhakikishe usalama.

1. Jina la kwanza la Mwanafunzi (likiwa limeandikwa vizuri)
2. Jina la Mwisho la Mwanafunzi (likiwa limeandikwa vizuri)
3. Shule ambayo mwanafunzi amepewa.
4. Tarehe ya Kuzaliwa ya Mwanafunzi
5. Nambari ya Kitambulisho cha Mwanafunzi, aliyopewa na wilaya ya shule.

**S: Jina la kwanza na la mwisho la mwanafunzi wangu huandikwa vibaya mara kwa mara au lina tahajia nyingi. Ni tahajia gani ninapaswa kutumia ili kufikia maelezo yake katika programu?**
J: Lazima utumie tahajia ya jina la kwanza na la mwisho ambayo inalingana na tahajia iliyotumiwa na mfumo wa maelezo ya mwanafunzi ya wilaya ya shule.

**S: Nina tatizo la kupata shule ya mwanafunzi wangu ya kujaza katika sehemu ya SHULE. Ni nini ninachokosa?**
J: Kuna njia mbili za kuchagua shule ya mwanafunzi wako.

1. Ya kwanza ni kutafuta kulingana na jila la shule. Unapokuwa ukiandika sehemu ya jina la shule, utaona shule ambazo zinalingana na jina hilo, kwa ukamilifu au kwa sehemu. Kwa mfano, kwa Shule ya Booker T. Washington, unaweza kuanza kwa kuandika “Booker” au “Washington” na orodha ya shule zinazolingana itatokea.

2. Njia nyingine, unaweza kubofya kwenye ikoni ndogo ya ramani upande wa kulia mwa sehemu ya shule na kisha upate shule kwenye ramani, na uchague ikoni iliyoonyeshwa katika eneo la shule.

**S: Mwanafunzi wangu anaonekana kama ANASUBIRI au AMEKATALIWA. Nifanye nini?**
J: Kwa kawaida, usajili wa mwanafunzi huonekana kama ANASUBIRI au AMEKATALIWA ikiwa sehemu zote 5 za usalama hazilingani. Unaweza kuona data ambayo uliweka kwa kuchagua mwanafunzi huyu katika programu na kukagua data ili uangalie makosa ya uchapishaji. Ikiwa una maswali kuhusu tahajia ya jina au nambari ya ID ya wilaya, unapaswa kuwasiliana na shule ya mwanafunzi.

**S: Ninawezaje kumfuta mwanafunzi kutoka kwa programu yangu?**
J: Kutoka kwenye kichupo cha WANAFUNZI, telezesha kushoto tu kwenye mwanafunzi huyo. Huu pia ndio mchakato unaotumia kufuta usajili wa ANASUBIRI au AMEKATALIWA.

## KUTUMIA PROGRAMU

**S: Kichupo cha MWANZO kinaniambia nini?**
J: Kichupo cha MWANZO huonyesha maelezo ya kawaida ya safari kwa kila mwanafunzi ambaye umemwongeza kwenye programu yako. Kwa kawaida hii itakuwa ni safari ya asubuhi na ya jioni. Kwa kila safari programu itaonyesha jina la mwanafunzi, kama arifu zimewashwa kwa safari hiyo, saa zilizoratibiwa za kumchukua na kumrudisha mwanafunzi na nambari ya basi. Safari huonyeshwa kwa mpangilio wa saa inayofuata ya kumchukua au kumrudisha mwanafunzi.

**S: Ikoni ya bahasha juu kulia mwa Skrini ya mwanzo ni nini?**
J: Idara ya usafiri ya wilaya ya shule yako inaweza kutuma ujumbe kwa wazazi na wengine ambao wanatumia programu hii. Ujumbe unaweza kutumwa kwa watu mahsusi au wale walio na wanafunzi waliopangiwa njia maalum ya basi. Watumiaji wa programu hupokea ujumbe huu kama arifu kwenye simu zao. Kuchagua ikoni ya bahasha hukuwezesha kuona ujumbe uliopokewa zamani.

**S: Saa za kuchukuliwa na kurudishwa humaanisha nini? Ni vipi kuhusu umbali?**
J: Kwenye kichupo cha MWANZO au skrini ya Ratiba ya Usafiri, maeneo na saa za kuchukuliwa na kurudishwa ni zile zinazopangwa na wilaya ya shule. Ikiwa wilaya itadumisha ratiba za kipekee za usafiri kwa siku tofauti za wiki, maelezo hayo yaliyopangwa hutokea hapa pia. Kwenye kichupo cha BASI LANGU, kuna umbali ambao unaashiria ni wapi basi liko, kunguru akipaa, kutoka kwa kituo kilichopangwa cha basi.

**S: Kuna tarehe na saa iliyoonyeshwa na ikoni ya basi. Hiyo inamaanisha nini?**
J: Kwenye kichupo cha BASI LANGU, saa iliyoripotiwa ya basi ya shule huonyeshwa kando ya ikoni ya basi.
**KUMBUKA**: Watumiaji wa programu wanapaswa kuelewa kwamba ikiwa eneo la basi halijaripotiwa hivi karibuni, huenda kukawa na matatizo na ishara ya GPS au matatizo mengine ya mawasiliano. Katika hali kama hiyo, wanafunzi wanapaswa kuripoti kwa kituo chao cha basi kwa saa za kawaida, dakika 5 kabla ya saa inayotarajiwa ya basi. Onyesho hili la saa ni muhimu ili kuwasaidia wazazi kufasiri kwa usahihi maelezo ya Basi Langu Liko Wapi.

**S: Kwa nini siwezi kuona eneo la basi letu la shule?**
J: Wilaya ya shule ina hiari ya ni lini wataruhusu ikoni ya basi kuonekana kwenye ramani. Wilaya nyingi huchagua kuonyesha ikoni ya basi wakati mabasi yako njiani tu.

**S: Itakuwa aje ikiwa ramani sio sahihi?**
J: Programu ya wazazi ya Edulog hutumia Ramani za Google kama ramani yake msingi ya kuonyeshana. Hakuna chanzo cha ramani ambacho ni kamili, lakini tumepata data katika Ramani za Google kuwa sahihi vya kutosha ili kuunga mkono programu hii. Kwa bahati mbaya, Edulog haina uwezo wa kusahihisha mara moja ramani ya Google. Unaweza kutoa maelezo moja kwa moja kwa Ramani za Google kupitia chaguo lao la "tuma maoni" https://www.google.com/maps.

**S: Iwapo mwanafunzi wangu atahamia basi lingine. Programu hii itashughulikia aje suala hilo?**
J: Shule ambayo umeweka ili kufikia data ya mwanafunzi ndio shule ambayo anahudhuria. Huenda ikawa amehamia basi la pili kabla ya kuwasili shuleni. Hata hivyo, arifu za asubuhi hutumwa basi likiwasili katika kituo cha basi ya shule cha "nyumbani". Hiyo ni kumaanisha, utaona eneo la basi ambalo linamchukua mwanafunzi katika kituo asili cha mabasi, yamkini karibu na nyumba. Vivyo hivyo, jioni utaona basi likikaribia kituo cha basi cha "nyumbani" na upokee arifu basi likikaribia kituo hicho.

**S: Tulihama (katika au ndani ya wilaya). Ni lini ninaweza kuanza kutumia programu?**
J: Muda wa kuanzisha ni juu ya wilaya ya shule yako. Huenda ikapatikana siku baada ya kubadilisha au ndani ya siku 2-3 ya ratiba iliyotekelezwa na wilaya.

## KUPOKEA ARIFU




**S: Ninawezaje kuarifiwa wakati mwanafunzi wangu ameingia au kushuka basi?**
J: Kuweka zoni za taarifa katika programu hukuwezesha kupokea arifu wakati basi linaingia zoni hiyo ambayo umefafanua katika kituo cha basi cha mwanafunzi wako. Zoni ya taarifa inapatikana katika kituo cha basi na inaweza kuwa na umbali wa maili 0 hadi 2. Arifu huwekwa na zoni zinaundwa chini ya kichupo cha MIPANGILIO. Arifu hutegemea kituo cha basi. Baadhi ya wilaya zinatoa arifu wakati wanafunzi "wanapanda" au "kushuka" basi wakitumia kadi. Maelezo haya yanahifadhiwa kwenye chaguo la "MTOTO WANGU YUKO WAPI" kwenye kichupo cha MWANAFUNZI.

**S: Ni wakati gani nitapata arifu basi likiwasili katika kituo cha basi?**
J: Unaweza kupokea arifu za kituo cha basi asubuhi au kituo cha basi jioni au zote. Weka zoni ya taarifa kwa kila moja. Kila moja inaweza kuwa na umbali tofauti. Iweke kwa ile ambayo inafaa zaidi kwa kila njia ya basi. Isitoshe, kuna muda wa arifu ambao una udhibiti pia. Muda chaguo-msingi ni kuanzia saa moja kabla hadi saa moja baada ya saa iliyoratibiwa ya kituo cha basi. Unaweza kuweka muda "mdogo", hasa ikiwa basi hilo moja liko katika eneo lako, pengine likihudumia shule nyingine, kabla au baada ya njia ya basi lako.

**S: Arifu hizi zinaweza kutegemewa?**
J: Arifu hizi hutumwa mara moja wakati ishara ya GPS kutoka kwa basi lako inapatikana ndani ya zoni ya arifu. Basi la shule hutuma ishara za mara kwa mara za GPS kwenye hifadhidata ya programu katika wingu kila sekunde 10-20. Kama vile teknolojia zote, ukatizaji unaweza kufanyika. Ucheleweshaji unaweza ukatokea iwapo kuna ukatizaji katika huduma ya simu au kifaa cha GPS kwenye basi kimetenganishwa. Hakikisha unafuatilia programu kwa mwenendo wa basi kabla ya saa inayotarajiwa ya basi.

## KUHUSU MAELEZO

**S: Programu nyingine zinaweza kutumia maelezo ya mwanafunzi wangu?**
J: HAPANA Watu walio na maelezo katika sehemu zinazohitajika za usalama tu ndio wanaweza kufikia maelezo ya usafiri ya mwanafunzi katika programu.

**S: Maelezo kuhusu kituo changu cha basi yanatoka wapi?**
J: Saa na eneo lililopangwa la kituo cha basi cha mwanafunzi wako zinatoka kwa mfumo wa usimamizi wa njia wa Edulog unaotumiwa na mtoa huduma wako wa usafiri wa shule.

**S: Picha ya mtoto wangu imehifadhiwa kwenye intaneti?**
J: HAPANA Picha ambazo unahusisha na programu, aidha kutoka kwa maktaba yako ya picha au zilizopigwa upya kwa kamera husalia kwenye kifaa chako cha mkononi ambacho ulianzisha programu. Ukipakia picha kwenye vifaa viwili tofauti, utahitaji kuhusisha picha kwenye kila kifaa.